



SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 2
SOUAHÉLI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2
SUAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2

Tuesday 2 November 2010 (morning)

Mardi 2 novembre 2010 (matin)

Martes 2 de noviembre de 2010 (mañana)

1 h 30 m

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not turn over this examination paper until instructed to do so.
- Choose one task.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne retournez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Choisissez une tâche.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No dé la vuelta al examen hasta que se lo autoricen.
- Elija una tarea.

Kamilisha mojawapo wa kazi zifuatazo kwa angalau maneno 400.

1. Kama mmojawapo wa wanafunzi wanaomaliza shule mwishoni mwaka huu umeombwa na darasa lako kutoa hotuba kwenye karamu yao ya kufuzu mwishoni mwa mwaka kuhusu jinsi ambavyo vijana wanaweza kutumia elimu yao siku za baadaye kulijenga taifa bora. Andika hotuba yako.
2. Maporomoko ya kiuchumi yaliyotokea ulimwenguni kote hivi karibuni yaliathiri shughuli mbalimbali za kijamii na za kitaifa. Kutokana na yale ambayo unayasikia televisheni, redioni na yale unayoyasoma magazetini, andika insha kueleza jinsi maporomoko haya yalivyokuathiri wewe, jamii yako na shule yako.
3. “Michezo huwa muhimu kwa ujenzi wa afya.” Wewe ukiwa kiranja wa michezo shulenii mwako umealikwa kwa mdahalo au majadiliano kuunga mkono kauli hii. Huku ukitoa mifano, itetee kauli hii.
4. Hivi karibuni kumekuwa na malalamiko kuhusu ongezeko la visa vyta uhalifu ndani ya shule yako na maeneo yaliyoko karibu nayo. Wewe ukiwa mmojawapo wa viongozi shulenii mwako umeombwa na gazeti la shule yako kuandika makala kuhusu chanzo cha uhalifu huu na njia mbalimbali ambazo zinaweza kutumiwa kuukomesha. Andika makala yako.
5. Mwanafunzi kutoka shule jirani ambaye angependa kujiunga na mfumo wa IB amekuandikia barua pepe/e-meli kutaka maelezo zaidi kuhusu faida za mfumo huu. Huku ukitoa mifano, mwandikie barua pepe/e-meli ukielezea faida za mfumo huu.
6. Umealikwa na mojawapo wa stesheni za radio nchini mwako kufanya mahojiano na mmojawapo wa waandishi shupavu wa mashairi kuhusu nafasi ya mashairi katika kujenga maadili katika jamii. Huku ukirejelea baadhi ya vitabu vyake vyta mashairi ambavyo umevisoma mhoji kuhusu kauli hii. Si lazima ushairi uwe wa Kiswahili.